TANGAZO LA SERIKALI NA 679 La Tarehe 21/8/2020

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya vifungu vya 6(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO ZA ADA NA USHURU ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA ZA MWAKA 2020

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda za Mwaka 2020.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:

"ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi wa umma yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni kifusi, udongo, mchanga, kokoto, mawe na matofali;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"soko" maana yake ni eneo au soko liliotengwa na linalomilikiwa na Halmashauri kama soko;

"stendi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo;

"ushuru" maana yake ni maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada na ushuru

3.- (1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri

itakavyoelekeza.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

4. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada na ushuru

5.- (1) Muda wa kukusanya ada na ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ada na ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ada na ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Usimamizi wa Sheria Ndogo

6.- (1) Halmashauri inaweza kufunga biashara au kusimamisha uendeshaji wa shughuli yoyote ambayo itafanyika bila ya kuwa na leseni au kibali kinachotolewa na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala wake anaweza kukamata na kuzuia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa masharti ya Sheria Ndogo hii.

(3) Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama, itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ada au ushuru unaodaiwa, gharama za kuhifadhi mali au bidhaa, gharama za Mahakama na gharama za mnada.

(4) Wakala hataruhusiwa kukamata mali au bidhaa bila kupata idhini ya maandishi ya Mkurugenzi.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa bidhaa au mali iliyokamatwa chini ya kifungu hiki isipokuwa tu kama uharibifu huo umesababishwa na Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

7.- (1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhini wa

8. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Makosa na adhabu

9.- (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii; au

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri shughuli zinazohitaji kulipiwa ushuru.

(2) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atahukumiwa adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne.

Kufifilisha kosa

10. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo

11.- Sheria Ndogo zifuatazo zinafutwa :-

Tangazo la Serikali Na. 266 la Mwaka 2008

(a) Sheria Ndogo za (Ushuru wa mazao) za Halmashauri ya Mji wa Mpanda za mwaka 2008 zinafutwa.

Tangazo la Serikali Na. 264 Mwaka 2008

(b) Sheria Ndogo za (Ushuru wa Masoko) za Halmashauri ya Mji wa Mpanda za mwaka 2008 zinafutwa.

Tangazo la Serikali Na. 265 la

(c) Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Mji wa Mpanda za mwaka 2008 zinafutwa;

| | | |
|---|---|---|
| Mwaka 2008 | | |
| Tangazo la Serikali Na. 318 la Mwaka 2010 | (e) | Sheria Ndogo za (Ushuru wa Kituo cha Magari ya Abiria na Mizigo) za Halmashauri ya Mji wa Mpanda za mwaka 2008 zinafutwa; |
| Tangazo la Serikali Na.272 la Mwaka 2008 | (f) | Sheria Ndogo za (Ushuru wa Nyumba/ Property Rates) za Halmashauri ya Mji wa Mpanda za mwaka 2008 zinafutwa; |

JEDWALI LA KWANZA
*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 3(1))*

SEHEMU YA KWANZA

1. Ada ya kukodi mali za Halmashauri

(i) Kukodi ukumbi wa Halmashauri kwa ajili ya mikutano/vikao ……………….……. Sh. 200,000/= Kwa siku
(ii) Kukodi viti …………………………………………………….…………….…Sh. 1,500/= Kwa kila kiti
(iii) Mitambo (trekta, total station, vifaa vya GPS na kadhalika) ……………..………... Kulingana na bei ya soko

2. Kodi ya vibanda vya biashara
(a) Vibanda kwenye Masoko ya Manispaa Mjini …...…………………………………... Sh. 50,000/= kwa mwezi
(b) Maeneo mengine ya Manispaa nje ya Mji ……………………………………...… Sh. 30,000/= kwa mwezi
(c) Kodi ya vibanda vya stendi ya mabasi Ilembo ………………………………….…. Sh. 100,000/= kwa mwezi
(d) Kodi ya *supermarket* stendi ya mabasi Ilembo ……………………………………... Sh. 350,000/= kwa mwezi
(e) Kodi ya vyumba mbalimbali vya biashara ……………………………………….…. Kulingana na bei ya soko.

SEHEMU YA PILI

1. Ushuru wa Soko na Minada
a) Meza/kizimba kwa sokoni ………………………………………………………………....  Sh. 300/= kwa siku
b) Wanaopanga bidhaa chini ……………………………………………………….……….... Sh. 300/= kwa siku
c) Tenga la samaki kwa wachuuzi sokoni ……………………………………………….…. Sh. 2,500/= kwa siku

*Tangazo La Serikali Na.. 679 (Linaendelea.).*

d) Tenga la nyanya/machungwa/limao ………………………………………………………. Sh. 300/= kwa siku

2. Ushuru wa minada;
(a) Meza ……………………………………………………………………………….… Sh. 1,500/= kwa siku

(b) Wauza mitumba/nguo …………………………………………………......…………… Sh. 1,500/= kwa siku

(c) Mamalishe …………………………………………………………………………...… Sh. 1,500/= Kwa siku

(d) Vinywaji ……………………………………………………………….………………. Sh. 1,500/= Kwa siku

(e) Biashara ndogo ndogo ………………………………………………………….……… Sh. 1,500/= Kwa siku

(f) Pombe za asili ………………………………………………………………………… Sh. 1,500/= Kwa siku

3. Ushuru wa Mnada wa mifugo;

(a) Ushuru wa Ng'ombe ……………………………………………….………. Sh. 4,000/= kwa kila mmoja.

(b) Ushuru Mbuzi, Kondoo, Nguruwe ....……………………………….…... Sh. 2,000/= kwa kila mmoja.

(c) Kuku/ Kanga/ Bata/Njiwa ……………………………………………………. Sh. 1,500/= kwa tenga moja.

(i) Jedwali la Orodha ya Minada na tarehe inayofanyika ndani ya Halmashauri;

| Na. | MNADA | KIJIJI | KATA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | Kakese | Mbugani | Kakese | Tarehe 5 na 20 ya kila mwezi |
| **2.** | Mwamkulu | Mwamkulu | Mwamkulu | Tarehe 8 na 22 ya kila mwezi |

(ii) Jedwali la Orodha ya Magulio na tarehe yanayofanyika ndani ya Halmashauri;

| Na. | GULIO | KIJIJI/MTAA | KATA | TAREHE YA GULIO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mpanda Hoteli | Majengo | Majengo | Kila wiki siku ya Jumapili |
| 2 | Stendi ya zamani | Mji Mwema | Kashaulili | Kila wiki siku ya Jumamosi |

SEHEMU YA TATU

3. Ushuru wa mazao;

*Tangazo La Serikali Na.. 679 (Linaendelea.).*

(a) Viazi ………………………………………….……………………………. 3% ya bei ya mauzo.

(b) Kabichi ……………………………………………………….……………. 3% ya bei ya mauzo.

(c) Karoti ……………………………………………………………………. 3% ya bei ya mauzo.

(d) Mchele………………………………………………………………………... 3% ya bei ya mauzo.

(e) Maharagwe/kunde...………………………………………………………... 3% ya bei ya mauzo.

(f) Vitunguu saumu ………………………………………………….………………… 3% ya bei ya mauzo.

(g) Vitunguu maji ……………………………………….………………….... 3% ya bei ya mauzo.

(h) Nyanya …………………………………………………………………………… 3% ya bei ya mauzo.

(i) Mahindi/Alizeti/Ngano/Mtama………………………………………………... 3% ya bei ya mauzo.

(j) Pumba za mahindi na mpunga ……………………………………………………… 3% ya bei ya mauzo.

(k) Mashudu ya alizeti na mengineyo ……………………………………...…... 3% ya bei ya mauzo.

(l) Nyasi za kulisha wanyama (hey) …………………………………………...…… 3% ya bei ya mauzo.

(m) Ufuta………………………………………………………………….…...... 3% ya bei ya mauzo.

(n) Pamba …………………………………………………………….……...… 3% ya bei ya mauzo.

(o) Tumbaku ……………………………………………………………………… 3% ya bei ya mauzo.

(p) Kahawa ……………………………………………………………………... 3% ya bei ya mauzo.

(q) Korosho ………………………………………………………………...…... 3% ya bei ya mauzo.

SEHEMU YA NNE

4. Ushuru wa Huduma za machinjio, Ukaguzi wa nyama, Ushuru wa bucha na Uchomaji.

(a) Ukaguzi kabla ya kuchinja

| NA. | MNYAMA | Ushuru |
|---|---|---|

*Tangazo La Serikali Na.. 679 (Linaendelea.).*

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 2000/= kwa mmoja |
| 2. | Mbuzi, Kondoo | 500/= kwa mmoja |
| 3. | Nguruwe | 500/=kwa mmoja |

(b) Ukaguzi baada ya kuchinja

| NA. | MNYAMA | Ushuru |
|---|---|---|
| 1) | Ng'ombe | 2000/=kwa mmoja |
| 2) | Mbuzi, Kondoo | 500/=kwa mmoja |
| 3) | Nguruwe | 500/=kwa mmoja |

(c) Kuuza na kuchoma Nyama mnadani……..……………………………………...… Sh. 1,500/= kwa siku.

(d) Kuuza na kuchoma Nyama, viazi n.k kwenye majiko …………………………………… Sh. 300/= kwa siku.

(e) Ushuru wa Bucha la Ng'ombe, Mbuzi, Kondoo, Nguruwe, na Samaki …………….……. Sh. 300/= kwa siku.

SEHEMU YA TANO

(a) Ada ya kibali cha kuendesha shughuli za Muziki na Michezo;

(i) Kibali cha kuchezesha disco la wazi ………………………………….….…… Sh. 15,000/= Kwa siku

(ii) Kibali cha kuchezesha disco ukumbini ……………………………….……. Sh. 20,000/= kwa siku

(iii) Kibali kwa ajili ya sherehe ……………………………………………….….... Sh. 20,000/= Kwa siku

(iv) Kibali cha kuchezesha mchezo wa FETE …....................................................… Sh. 60,000/= Kwa mwezi

(v) Kibali cha kuchezesha michezo ya kubahatisha....................................................Sh. 60,000/- kwa mwezi

(vi) Kibali cha kuendesha michezo ya utamaduni …………………………………... Sh. 50,000/= Kwa siku.

(vii) Kibali cha kupiga muziki kwa sauti eneo la biashara ..........................................Sh. 40,000/= kwa mwezi

(b) Ada ya uzalishaji wa pombe za asili;

*Tangazo La Serikali Na.. 679 (Linaendelea.).*

(i) Uzalishaji kwenye viwanda vidogovidogo ............................................ Sh. 30,000/= kwa mwezi mmoja.

(ii) Uzalishaji kwa mtu mmoja mmoja ………………………...…………. Sh. 1,000/= kwa kibali kimoja.

SEHEMU YA SITA

5. Ushuru wa Stendi, Maegesho na Usajili wa vyombo vya usafiri.

(a) Ushuru wa Maegesho ya vyombo vya usafir**i**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Pikipiki | Sh. 300/= kwa siku |
| 2. | Teksi | Sh. 500/= kwa siku |
| 3. | Lori chini ya tani 2/ Pick up | Sh. 500/= kwa siku |
| 4. | Lori chini ya tani 5/Fuso | Sh. 1,000/= kwa siku |
| 5. | Lori zaidi ya tani 5 | Sh. 1,500/= kwa siku |
| 6. | Magari mengine yasiyo ya biashara | Sh. 500/= kwa siku |

(b) Ushuru wa stendi

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa mtu kuingia stendi | Sh. 200/= kwa kuingia |
| 2. | Baiskeli | Sh. 200/= kwa kutoka |
| 3. | Pikipiki | Sh. 300/= kwa kutoka |
| 4. | Teksi/ Gari ndogo chini ya abiria 5 | Sh. 500/= kwa kutoka |
| 5. | Basi chini ya abiria 25 | Sh. 500/= kwa kutoka |
| 6. | Basi zaidi ya abiria 25 | Sh. 1,000/=kwa kutoka |
| 7. | Basi zaidi ya abiria 40 | Sh. 2,000/= kwa kutoka |

SEHEMU YA SABA

Ada na Ushuru wa Maegesho, Kupakia na kupakua mizigo, Usajili na Uoshaji wa vyombo vya usafiri.

(a) Ada ya Usajili wa vyombo vya usafiri na kutoa Stika,

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya usajili wa pikipiki ya magurudumu 3 (SUMATRA) | Sh: 32,000/= |
| 2. | Ada ya usajili wa pikipiki ya magurudumu 2 (SUMATRA) | Sh: 22,000/= |

(b) Ushuru wa Maegesho ya vyombo vya usafiri katika eneo lote la Halmashauri

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Pikipiki | Sh. 300/= kwa siku |
| 2. | Teksi | Sh. 500/= kwa siku |
| 3. | Lori chini ya tani 2/ Pick up | Sh. 500/= kwa siku |
| 4. | Lori chini ya tani 5/Fuso | Sh. 1,000/= kwa siku |

*Tangazo La Serikali Na.. 679 (Linaendelea.).*

5. Lori zaidi ya tani 5 — Sh. 1,500/= kwa siku
6. Magari mengine yasiyo ya biashar — Sh. 500/= kwa siku

(c) Ushuru wa magari yanayoingia kupakia na kupakua mizigo maeneo ya Miji.

1. Lori/gari la tani 1 – $3^1/_2$ — Sh: 5,000/=
2. Lori la tani 4 -7 — Sh: 10,000/=
3. Lori la tani 8 hadi 10 — Sh: 15,000/=
4. Lori zaidi ya tani 10 — Sh. 50,000/=

SEHEMU YA NANE

7. Ushuru wa madini ya ujenzi.

MAWE, KIFUSI, MCHANGA, TOFARI NA KOKOTO**.**

| | | |
|---|---|---|
| 1) | Gari ya tani 1 – 3½ | Sh: 5,000/= kwa safari moja |
| 2) | Gari ya tani 4 – 7 | Sh: 10,000/= kwa safari moja |
| 3) | Gari ya tani 8 na kuendelea | Sh: 20,000/= kwa safari moja |
| 4) | Mkokoteni wa kuvutwa na binadamu | Sh: 1,000/= kwa safari moja |
| 5) | Mkokoteni wa kuvutwa na wanyama kazi | Sh: 10,000/= kwa safari moja |

SEHEMU YA TISA

8.Ada ya shughuli za ujasiliamali na Vibali vya kufanya biashara

(a) Ada ya utafiti wa madini itakuwa ni Sh. 500,000/= kwa kibali kwa hekta moja.
(b) Ada ya kuendesha kraha ya kuchaka madini/maduara ni Tshs. 100,000/= kwa mwaka.
(c) Ada ya kibali cha kununua mazao ya chakula ni Sh. 200,000/= kwa msimu mmoja.
(d) Ada ya kibali cha kununua mazao ya biashara ni Sh. 500,000/= kwa msimu mmoja.
(e) Ada ya kibali cha kuhifadhi mazao ghalani ni Sh. 500,000/= kwa msimu mmoja.

SEHEMU YA KUMI

9. Ada ya kibali cha kuweka matangazo ya biashara

| Aina ya tangazo | | Kiwango cha ada |
|---|---|---|
| (i) | Maombi ya kuweka mabango ya Biashara/kuchora | Sh. 10,000/= |
| (ii) | Matangazo yanayong'aa (yanayowaka kwa nguvu ya umeme) kwa mita ya mraba kwa mwaka | Sh. 30, 000/= Kwa mwezi |
| (iii) | Ubao wa tangazo usioangaza kwa mita ya mraba | Sh. 20,000/= Kwa mwezi |
| (iv) | Kodi ya pango (kwa mabango au mbao zisio za matangazo | Sh. 20,000/= Kwa mwezi |

*Tangazo La Serikali Na.. 679 (Linaendelea.).*

(v) Matangazo kwa njia ya maonesho

| | |
|---|---|
| (a) Kutambulisha bidhaa | Sh. 15,000/= Kwa siku |
| (b) Kutambulisha huduma | Sh. 15,000/= Kwa siku |

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

Ada ya Vibali vya ujenzi

1. Kibali cha ujenzi kwa nyumba za makazi pekee.…………………………………….………... Tsh. 50,000/=.

2. Kibali cha ujenzi kwa nyumba za makazi na biashara …………………………….…….……Tsh. 100,000/=.

3. Kibali cha ujenzi kwa nyumba za biashara pekee ……………………………….……….…... Tsh. 200,000/=.

4. Kibali cha ujenzi kwa eneo la ujenzi wa ghala ……………………………………….………Tsh. 200,000/=.

5. Kibali cha ujenzi kwa nyumba ya ghorofa ……………………………………………….…... Tsh. 500,000/=.

6. Kibali cha ujenzi kwa ajili ya kituo cha kuuzia mafuta .......................................................... Tsh. 2,000,000/=.

7. Kibali cha ujenzi kwa ajili ya kiwanda kidogo ....................…………………………...……... Tsh. 500,000/=.

8. Kibali cha ujenzi kwa ajili ya kiwanda kikubwa …………………………………….……..... Tsh. 750,000/=.

9. Kuidhinisha marekebisho ya ramani/michoro ya jengo ……………………………….……….…Tsh. 20,000=.

10. Kibali cha nyongeza na mabadiliko katika jengo lililokamilika …………………………………Tsh. 30,000/=.

11. Kibali cha kubadili matumizi ya eneo itakuwa 50% ya kiwango cha kibali husika kulipiwa.

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 10)*

KUFIFILISHA KOSA

Mimi…………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda kuwa tarehe ………mwezi………. Mwaka………. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha………………. cha Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ya Mwaka, 2020.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, nipo tayari kulipa shilingi laki mbili na kutimiza wajibu wangu chini ya Sheria Ndogo hiyo badala ya kushtakiwa mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………………. ya Mwezi…………………. Mwaka…………………

Jina……………………………………………...…Saini……………………………

Mbele ya:

Jina………………………………………...Cheo……………………………………

Saini……………………………………Tarehe…………………………………...

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa imegongwa katika sheria Ndogo hizi kufuatia azimio Na: MUHT/MMC/BARAZA/02/2018/2019/AGD:13 la kikao cha Halmashauri ya Manispaa Mpanda kilichofanyika tarehe 25 Januari, 2019, na kimebandikwa na kushuhudiwa na;

MICHAEL F.NZYUNGU
*Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Manispaa Mpanda*

*WILLIAM P. MBOGO*
*Mstahiki Meya*
*Halmashauri ya Manispaa Mpanda.*

**L.S**

NAKUBALI

Dodoma
5 Agosti,2020

SELEMANI S. JAFO (MB)
*Waziri wa Nchi,*
*Ofisi ya Rais,*
*Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*